WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 57 | July 1 - 21 2024



# RAIS SAMIA ATAKA WIZARA YA NISHATI KUONGEZA KASI USIMAMIZI WA MIRADI

WIZARA YA NISHATI   +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**
Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**
Dkt. James Mataragio

**MHARIRI**
Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**
Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya

**WAPIGA PICHA**
Steven Nyamiti
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana

**MSANIFU KURASA**
Brian Mbaga


© NISHATI 2024

# RAIS SAMIA ATAKA WIZARA YA NISHATI KUONGEZA KASI USIMAMIZI WA MIRADI

- Lengo ni kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati
- Aeleza umeme unavyochagiza shughuli za kiuchumi
- Vijiji 621 Morogoro vyafikiwa na umeme kati ya Vijiji 669



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiongea na wananchi wa Mkoa wa Morogoro wakati wa ziara yake ya kikazi ya kutembelea na kukaguwa miradi mbalimbali ya maendeleo, tarehe 06 Agosti 2024.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiagiza Wizara ya Nishati kuongeza nguvu katika kusimamia miradi yote ya nishati ili ikamilike kwa wakati na hivyo kuwawezesha wananchi kupata nishati ya uhakika.

Rais Samia ametoa agizo hilo Agosti 06, 2024 wakati akihitimisha ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro.

"Nimejionea mwenyewe wakati naenda Kilosa tofauti iliyokuwa ikionekana maeneo ambayo hayana umeme na yale yenye umeme ambayo yameshamiri kwa shughuli za biashara, hii inaonesha umuhimu wa nishati katika maeneo yote nchini." Amesisitiza Dkt.Samia

Aidha, Rais Samia ameutaka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kukamilisha mapema kupeleka umeme kwenye Vijiji vilivyobaki na kuongeza kasi ya kusambaza umeme kwenye Vitongoji ili wananchi waweze kufanya kazi za maendeleo.

Aidha, amesisitiza kuwa uwepo wa umeme wa uhakika kutoka Bwawa la Julius Nyerere kunaufanya Mkoa wa Morogoro kuwa sehemu sahihi ya uwekezaji.

"Morogoro sasa ina umeme wa uhakika, hali inayovuta uwekezaji ndani ya Mkoa." Ameongeza Mhe. Rais

Akizungumzia kuhusu miradi ya umeme vijijini Mkoa wa Morogoro, Dkt. Samia amesema kupitia Wakala wa Nishati Vijijini Serikali imepeleka umeme kwenye Vijiji 621 kati ya Vijiji 669.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akipokea maelekezo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro mara baada ya kutembelea na kukaguwa miradi ya maendeleo, tarehe 06 Agosti 2024.




Wananchi wa Mkoa wa Morogoro wakimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassani wakati wa mkutano wa hadhara wa kuhitimisha ziara yake ya kikazi mkoani humo, mara baada ya kutembelea na kukaguwa miradi mbalimbali ya maendeleo, tarehe 06 Agosti 2024.

# TANZANIA YAJIPANGA KUTUMIA NISHATI YA NYUKLIA KUZALISHA UMEME - DKT. BITEKO

- Asema mashapo 58,500 ya urani kutumika kama chanzo cha uzalishaji
- Marekani kuendeleza ushirikiano na Afrika matumizi Nishati ya Nyuklia




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko wakati akiwasilisha Mpango wa Tanzania katika Mkutano wa Pili wa Masuala ya Nishati ya Nyuklia kati ya Marekani na nchi za Afrika (US-Africa Nuclear Energy Summit) unaoendelea Jijini Nairobi, Nchini Kenya.

Tanzania imeeleza mpango na utayari wake katika uendelezaji wa nishati ya nyuklia ikiwa ni moja ya vyanzo mbadala vya nishati safi ya umeme kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko wakati akiwasilisha Mpango wa Tanzania katika Mkutano wa Pili wa Masuala ya Nishati ya Nyuklia kati ya Marekani na nchi za Afrika (US-Africa Nuclear Energy Summit) unaoendelea Jijini Nairobi, Nchini Kenya.

Katika mkutano huo unaojumuisha viongozi katika Sekta ya Nishati, Watunga Sera na Wataalam kutoka nchi mbalimbali barani Afrika, Dkt. Biteko amesema Tanzania iko tayari kuendeleza nishati ya nyuklia ikiwa ni moja ya vyanzo vitakavyoiwezesha nchi kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika na ambayo inakidhi viwango vya kimataifa katika uhifadhi wa mazingira.

"Utayari wa Tanzania katika kuendeleza na kutumia nishati ya nyuklia unatiliwa mkazo katika Sera ya Nishati ya mwaka 2015, Sera ya Madini ya mwaka 2009, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme na Mkakati wa Nishati Jadidifu ambapo nyaraka zote hizi zinatambua umuhimu wa nyuklia kukidhi mahitaji ya nishati nchini." Ameeleza Dkt. Biteko

Amesema chini ya uongozi wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali inaendelea kuchukua hatua muhimu zitakazowezesha matumizi ya nishati nyuklia kama moja ya vyanzo vya nishati safi ambapo hadi sasa Tanzania ina mashapo ya madini ya urani takriban tani 58,500 ambayo yanaweza kutumika kama chanzo

cha uzalishaji wa nishati ya nyuklia.

Amefafanua kuwa, uwepo wa vyanzo mbadala wa vya umeme utawezesha nchi kuboresha mashirikiano yake ya kibiashara na nchi nyingine ndani na nje ya bara la Afrika na hivyo kuboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Mpango huu wa kuwa na umeme wa kutosha utawezesha hatua ya kuunganisha gridi za umeme miongoni mwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika na baadaye katika maeneo mengine ya Bara hili." Amesema Dkt.Biteko

Ametumia mkutano huo kueleza nia ya Tanzania kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo nchi ya Marekani na Bara la Afrika ili kuendeleza nishati ya nyuklia hasa ikizingatiwa kuwa takriban watu milioni 600 barani Afrika na biashara ndogondogo zipatazo milioni 10 bado zinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Amesema mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanakua kwa asilimia 10 hadi 15 kwa mwaka na ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu, Tanzania imepanga kuzalisha megawati 10,000 za umeme ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wake, Msaidizi Maalum wa Rais wa Marekani wa Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira, Fedha na Uvumbuzi, Bw. Nana Ayensu amesema kuwa mkutano huo ni muhimu kwa nchi washiriki katika kufungua milango ya uendelezaji wa nishati ya nyuklia ambayo ni rafiki kwa matumizi ya binadamu na hifadhi ya mazingira na pia kuimarisha ushirikiano miongoni mwa nchi husika.

Ameongeza kuwa nishati ya nyuklia itafanikisha ajenda za kimataifa za nishati safi zinazoendelea ikiwemo nishati safi ya kupikia inayopigiwa chapuo kimataifa huku kinara wake akiwa ni Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Akizungujmzia utayari wa nchi yake, amesema Marekani ipo tayari kushirikiana na nchi za Afrika ili kuendeleza matumizi ya nishati ya nyuklia ambayo inatoa uhakika wa upatikanaji nishati na kuchochea maendeleo ya kiuchumi.



# GRIDI YA TAIFA INA UMEME WA KUTOSHA - RAIS SAMIA

- Kituo kikubwa cha umeme chajengwa wilayani Kongwa
- Kuimarisha umeme hadi Gairo

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema mfumo wa gridi ya Taifa una umeme wa kutosheleza mahitaji ya kijamii na kiuchumi.

Rais Samia ameyasema hayo leo Agosti 02, 2024 wilayani Gairo Mkoa wa Morogoro akiwa katika ziara ya kikazi.

Ameeleza kuwa, Serikali inazidi kuimarisha hali ya upatikanaji umeme nchini kupitia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ambapo imejenga kituo cha kupokea na kupoza umeme wilayani Kongwa mkoani Dodoma ambacho kitaboresha pia hali ya umeme wilayani Gairo.

Ameongeza kuwa, njia ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha kupoza umeme cha Kongwa kwenda wilayani Gairo imeshakamilika.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiongea na wananchi wa wilaya ya Gairo mkoani Morogoro wakati wa ziara yake ya kikazi ya kutembelea na kukaguwa miradi mbalimbali ya maendeleo, tarehe 02 Agosti 2024.




Mbunge wa Jimbo la Gairo Mhe. Shabibi akimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali katika jimbo hilo wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro




Wananchi wa wilaya ya Gairo wakimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro

# TAZAMA YATOA GAWIO BILIONI 4.35 KWA SERIKALI

- Dkt. Biteko asema ni matokea ya ziara ya Rais Samia nchini Zambia
- Aitaka TAZAMA ijiendeshe kwa faida




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (wa tatu kushoto) akimpongeza Msajili wa Hazina, Bw. Nehemiah Mchechu mara baada ya kupokea mfano wa hundi ya zaidi ya Shilingi Bilioni 4.35, kutoka Kampuni ya TAZAMA katika hafla iliyofanyika Agosti 26, 2024 jijini Dae es Salaam

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amepokea gawio la Serikali la zaidi ya Shilingi Bilioni 4.35, kutoka Kampuni ya Bomba la Kusafirisha Mafuta la Tanzania - Zambia (TAZAMA).

Dkt. Biteko amepokea gawio leo Agosti 26, 2024 jijini Dar es Salaam huku akishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa nchi hizo mbili ambapo ni miaka mitano tangu kutolewa kwa gawio mwaka 2019.

Amesema mapokezi ya gawio hilo ni matokeo ya ziara ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan nchini Zambia ambapo alielekeza miradi isimamiwe vizuri ili ilete matunda na kubadili maisha ya watu wa nchi hizo mbili.

"Nawapongeza sana Bodi ya TAZAMA na Wizara ya Nishati kwa hatua hii, haya ni matokeo ya ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Zambia ambapo alituelekeza miradi hii tuisimamie na ilete matunda na kubadili maisha ya watu wa nchi zetu." Amesema Biteko.

Aidha, ameitaka TAZAMA kuendelea kulisimamia vizuri Bomba hilo ili lizidi kuleta faida ambapo mikakati iliyopo sasa ni kuongeza ukubwa wa bomba la TAZAMA kutoka inchi nane hadi inchi 12.

Pia, amesema kuwa, Serikali

za nchi hizo mbili ziko katika hatua za manunuzi kwa ajili ya kujenga bomba kubwa la mafuta lenye kipenyo cha inchi 24, suala litakalopunguza gharama za usafirishaji wa bidhaa hiyo, ikiwa ni pamoja na kulinda miundombinu yake.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Prof. Kitila Mkumbo ameeleza kuwa Kampuni hiyo iliyokuwa kwenye hati ya kufa imeonesha kufufuka na kutoa gawio kwa Serikali.

"Tumezoea Watu na Mashirika yakiomba pesa kwa Serikali, lakini leo ni kinyume na tunashuhudia Serikali ikipokea gawio, hilo ni jambo la kujivunia sana." Amesema Prof. Mkumbo

Kwa upande wake, Msajili wa Hazina, Bw. Nehemiah Mchechu amesema kwa umri wa Kampuni ya TAZAMA yenye miaka 58 tangu kuanzishwa kwake imeonesha matumaini makubwa kwa kuanza upya kutoa gawio kwa Serikali na hii ni kutokana na utekelezaji wa 4R za Rais Samia Suluhu Hassan.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea mfano wa hundi ya zaidi ya Shilingi Bilioni 4.35, kutoka Kampuni ya TAZAMA katika hafla iliyofanyika Agosti 26, 2024 jijini Dae es Salaam

# RAIS SAMIA AMEIBEBA AJENDA YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KIMATAIFA - DKT. BITEKO

- Ashiriki Kongamano la Nishati Safi ya kupikia Zanzibar
- Ahamasisha ubunifu katika teknolojia za Nishati Safi ya Kupikia
- Apongeza ubunifu wa mita za kupimia gesi
- Wadau wahamasishwa kutoa elimu ya Nishati Safi ya Kupikia




Imeelezwa kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia nchini na Afrika bado anaendelea kuipeleka ajenda hiyo Kimataifa ili kuhakikisha watu wanapika katika mazingira salama kiafya na kimazingira.

Hayo yamebainishwa leo Agosti 23, 2024 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko katika Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia ambalo limeandaliwa na Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF) na Benki ya Uwekezaji ya Tanzania (TIB) kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zote za Serikali lililofanyika katika Hoteli ya Kwanza, Kizimkazi Zanzibar.

Amesema kuwa, suala la nishati safi ya kupikia imekuwa ni ajenda muhimu nchini na duniani kote na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa ni kinara wa ajenda hiyo Afrika kwa kuibeba kuanzia mwezi Novemba 2022.

Dkt. Biteko amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapika katika mazingira salama na kwamba hatua hii itawezekana kwa kupatikana kwa nishati safi ya kupikia iliyo nafuu, inayopatikana na kutumika kwa urahisi.

"Matarajio yetu ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Nimefarijika sana kuona utekelezaji wa lengo hili kwa vitendo, nimeona teknolojia mbalimbali katika mabanda ya maonesho hapo nje na niendelee kuhamasisha ubunifu wa teknolojia zinazowezesha wananchi

kupata nishati safi kwa gharama nafuu." Amesema Dkt. Biteko

Amesema Wizara ya Nishati itaendelea kutoa kipaumbele ajenda hiyo kwa namna mbalimbali ikiwemo kuanzisha Kitengo maalum cha usimamizi wa nishati hiyo.

Vile vile, Dkt. Biteko amewapongeza wabunifu kutoka banda la ORXY ambao wamekuja na ubunifu kwenye mitungi ya gesi (LPG) kwa kuweka mita inayopima gesi ambayo inarahisisha gharama za kujaza gesi na kuwa nafuu zaidi.

Pia, ametoa wito kwa viongozi wote wa Serikali, Siasa, Dini na wa Jadi waliopo katika maeneo mbalimbali kuunga mkono ajenda hiyo yenye nia njema ya kumkomboa kila Mtanzania na kwamba kwenye majukwaa yao, wasiliache nyuma suala hilo.

"Tuhakikishe watu tunaowaongoza wanaelewa vyema umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kwa kampuni zinazowajibika katika jamii zao kupitia Corporate Social Responsibilities (CSR) niwahimize kushirikiana na Serikali katika kutekeleza Mkakati kwa vitendo kwa kugawa vifaa vya nishati safi ya kupikia kwa wenye uhitaji. Naamini tukishirikiana wote kwa pamoja tutaweza." Amesema Dkt. Biteko.

Halikadhalika amesema, takriban watu bilioni 2.4 hawatumii nishati safi duniani, kati ya hao milioni 933 wanatoka Afrika na kwa mwaka duniani watu milioni 3.7 wanakufa na vifo ni asilimia 60 wakiwemo wanawake na watoto.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Mhe. Ayoub Mohammed Mahamoud, amesema suala la Nishati Safi ya Kupikia sasa ni ajenda ya Kimataifa na wataibeba katika






kutoa elimu na kuelimisha umma kususu matumizi salama ya nishati hiyo kwa upana

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF), Wanu Hafidh Ameir amesema Nishati safi ya Kupikia imekuwa ni mkombozi kwa wanawake na kulinda Afya zao.

Amewataka watanzania kutumia nishati hiyo ambayo ni mkombozi wa utunzaji wa mazingira na kiuchumi nchini.

Tamasha la Kizimkazi mwaka 2024, limesheheni vitu vingi ikiwemo ufunguzi wa miradi mbalimbali ikiwemo kiwanja cha Suluhu Academy.

# TANZANIA IPO TAYARI KUTUMIA FURSA YA SOKO LA PAMOJA KUUZIANA UMEME - DKT. BITEKO

- Ni kufuatia uwepo wa fursa hiyo kwa nchi 13 wanachama wa EAPP
- Mawaziri waridhia uwepo wa kitengo huru cha masoko cha kuuziana umeme
- Wanachama EAPP watachangia Megawati Elfu 90 kwenye soko la pamoja la kuuziana umeme




Tanzania imejipanga vema kuhakikisha inatumia fursa ya uwepo wa soko la pamoja la mauziano ya umeme kwa nchi wanachama wa soko la pamoja la nchi za Mashariki mwa Afrika (East African Power Pool)- EAPP kwa kuhakikisha inaunganisha miundombinu yake ya kusafirisha umeme na nchi wanachama wa EAPP.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko wakati wa mkutano wa 19 wa nchi wanachama wa umoja wa mauziano ya umeme EAPP uliowakutanisha Mawaziri wa Nishati na Makatibu Wakuu nchini Uganda.

Mkutano huo umezungumzia masuala mbalimbali ikiwemo kupitisha mabadiliko ya muundo wa kiuongozi wa EAPP, kuridhia kanuni na taratibu za kiuendeshaji za EAPP sambamba na kuridhia uwepo wa kitengo huru cha masoko kinachojitegemea kusimamia soko la pamoja la mauziano ya Umeme kwa nchi wanachama.

"'Nafurahi kuona kuwa tumefikia muafaka kwenye masuala ya msingi kwenye kikao cha Mawaziri wa Nishati hususani uwepo wa kitengo huru cha Masoko kinachojitegemea kwa ajili ya kusimamia mauziano ya umeme na kwakuwa Tanzania tutakuwa na umeme kutoka mradi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere -JNHPP, tutatumia vema fursa hiyo kuwauzia umeme nchi wanachama pale tutakapokuwa na ziada na sisi kununua tutakapokuwa na upungufu" amesema Dkt. Biteko.

Katika kufanikisha hilo Dkt. Biteko amesema tayari miundombinu wezeshi inaendelea kuwekwa kupitia Shirika la Umeme Tanzania TANESCO ili kujiandaa kuingia kwenye soko la pamoja ambapo laini kubwa ya kuunganisha Tanzania na Kenya kupitia Namanga imeshajengwa na imekamilika na ile ya kuunganisha Tanzania na Zambia-TAZA imeshaanza kujengwa na itakamilika ifikapo 2026.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa sasa wa soko la pamoja la kuuziana umeme la nchi za kaskazini Mashariki EAPP na Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Madini nchini Uganda Mhe. Dkt.

Aidha, Mhe Ssentamu amesema maadhimio hayo yamefikiwa kufuatia makubaliano ya mkutano wa 18 wa baraza la mawaziri ulioanyika nchini Kenya kuhusu umuhimu wa kupitia mapendekezo ya uendeshaji wa shughuli za EAPP.

Naye, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba amesema pindi uuzaji wa umeme kwenye soko la pamoja utakapoanza utatoa nafasi za ajira kwa nchi wanachama wa EAPP pamoja na kubadilishana wataalamu hususan kwenye miradi ya kusafirisha umeme na hivyo kuiongezea TANESCO mapato na hatimae kutoa nafasi ya ukuaji wa pato la Taifa.

Mtendaji wa TANESCO Mha. Gissima Nyamo-Hanga, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Mipango, Utafiti na Uwekezaji TANESCO CPA Renata Ndege, viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.




Ruth Ssentamu amesema EAPP imeridhia ushiriki wa Makatibu Wakuu wa Nishati kutoka nchi wanachama kushirikishwa katika muundo wa kiutawala wa EAPP kwa ajili ya kusaidia kuchakata na kupitia taarifa kutoka kwa watendaji wa kisekta kabla ya kupelekwa katika kikao cha baraza la Mawaziri la nchi wanachama ili kutolewa maamuzi.

Ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo wa Baraza la Mawaziri wa Nishati uliongozwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Mhe. Dennis Londo, Katibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba, Mkurugenzi

# TANZANIA MWENYEJI MKUTANO WA MAFUTA NA GESI MACHI 2025

- Wadau Sekta ya Nishati zaidi ya 1000 kushiriki
- Dkt. Biteko awataka wadau kushirikiana kuelekea mkutano huo
- Nishati Safi ya kupikia kupewa kipaumbele



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameshiriki katika kikao cha maandalizi ya Mkutano na Maonesho ya 11 ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) unaotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 5 hadi 7 Machi, 2025 katika ukumbi wa JNICC jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo wa siku tatu wa kimataifa utafanyika chini ya kauli mbiu "Unlocking Investment in Future Energy: The Role of Petroleum Resources in the Energy Mix for Sustainable Development in East Africa" ambapo utatanguliwa na kufuatiwa na safari za kutembelea maeneo ya kijiolojia na kujionea vivutio mbalimbali kitalii vilivyopo katika nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Aidha, watazungumzia masuala ya mabadiliko kuelekea katika matumizi ya nishati safi na kuwakutanisha wadau zaidi ya 1000 kutoka mataifa mbalimbali wanatarajiwa kushiriki katika mkutano huo.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Biteko alisema "Kama nchi tumepata fursa ya kuandaa mkutano huu wa kimataifa na Serikali imepanga kufanya hivyo kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuandaa mkutano wenye tija kwa nchi na kutoa nafasi kwa Watanzania kufaidika na uwepo wa mkutano huu".

Dkt. Biteko alitoa rai kwa wahudhuriaji wa kikao hicho kutumia vema fursa ya uwepo wa mkutano wa EAPCE'25 kutangaza biashara, huduma na utaalamu wao pamoja na kujenga mitandao na washirika kutoka mataifa mbalimbali.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba alieleza kuwa mkutano wa EAPCE'25 pia utahusisha maonesho ya huduma na bidhaa mbalimbali na hivyo kutoa fursa kwa wadau kuchangamkia fursa hiyo.

"Sambamba na mkutano na maonesho eneo lingine ambalo wadau wanakaribishwa kuchangamkia ni udhamini wa mkutano ambao unatoa nafasi ya kujitangaza ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia ukubwa wa mkutano wenyewe" alisema Mha. Mramba.

Kikao hicho ni cha awali cha maandalizi kuelekea mkutano wa EAPCE'25. Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti (www.eapce25.eac.int)








# RAIS SAMIA ARIDHIA VITUO 75 VYA KUPOZA UMEME KUJENGWA NCHINI - KAPINGA

- Lengo ni kuimarisha upatikanaji umeme katika maeneo yote nchini
- Mradi kugharimu shilingi Trilioni 4.42
- Vituo nane vyakamilika; sita vipo asilimia 97



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo yanayousu ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Ifakara kutoka kwa Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga wakati wa ziara yake Mkoani Morogoro alipotembelea kituo hicho tarehe 04 Agosti 2024.

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan ameridhia Wiizara ya Nishati kupitia TANESCO kujenga vituo 75 vya kupokea, kupoza na kusambaza umeme ikiwa ni jitihada zake za kuhakikisha wananchi katika maeneo yote wanapata umeme wa uhakika.

Mhe. Kapinga amesema hayo Agosti 04, 2024 wakati wa ziara ya Rais, Mhe. Dkt. Samia katika kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Ifakara mkoani Morogoro.

"Kabla ya mwaka 2021 nchi ilikuwa ina vituo 61 tu vya kupokea na kupoza umeme, tunakushukuru sana Mhe. Rais kwa kuridhia ujenzi wa vituo vingine vipya 75." Amesema Mhe. Kapinga

Kapinga ameeleza kuwa, ujenzi wa vituo hivyo vipya utagharimu takribani shilingi Trilioni 4.42 ambapo mradi huo unatekelezwa kwa awamu.

Ameongeza kuwa, katika mradi huo tayari vituo nane vimejengwa na kuanza kazi huku vituo sita vikifikia asilimia 97.


Akizungumzia ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ifakara, Kapinga amesema kuwa, kimeleta tija kwani kwa kukamilika kwake licha ya kupeleka umeme wa uhakika kwa wananchi, kimewezesha takribani viwanda

vipya 54 kuunganishwa na huduma ya umeme.

Akizungumzia kuhusu miradi ya kuiunganisha Tanzania na Nchi za Ukanda wa Mashariki mwa Afrika na Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika, amesema Rais Samia amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha Tanzania inaungana na nchi hizo kupitia miradi mbalimbali kama wa TAZA.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mha. Hassan Saidy amesema kituo cha Ifakara kimejengwa kutokana na uhitaji mkubwa wa umeme wilayani Ifakara, Malinyi na Ulanga na hii pia inatokana na shughuli kubwa za kilimo na uchimbaji madini.

Mha. Hassan ameongeza kuwa, kabla ya ujenzi kituo cha Ifakara umeme kwa mwezi ulikuwa ukikatika mara 18 ambapo hivi sasa ikitokea umeme umekatika basi ni mara moja.



Muonekano wa kituo cha kupoza umeme cha Ifakara wakati wa ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu mkoani Morogoro alipotembelea kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Ifakara, Tarehe 04 Agosti 2024.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mha Hassan Saidy wakati wa ziara yake mkoani Morogoro alipotembelea kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Ifakara, Tarehe 04 Agosti 2024.

# SHILINGI BILIONI 4.6 KUPELEKA UMEME MAENEO YA MIGODI RUVUMA - KAPINGA

- Asema Serikali itaendelea kupeleka umeme maeneo ya uwekezaji
- Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaj







Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Serikali imetenga takribani shilingi bilioni 4.6 kupeleka umeme kwenye maeneo ya migodi mkoani Ruvuma.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Agosti 18, 2024 wakati akizindua Kituo cha Mauzo ya Makaa ya Mawe ya kampuni ya Market Insight Limited (MILCOAL), inayojihusisha na uchimbaji, uuzaji na usambazaji wa Makaa ya Mawe, Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma.

"Hapa katika mgodi wa MILCOAL tutatumia takribani shilingi milioni 280 kuleta umeme, nguzo tayari zimeshawekwa na sasa hivi wataalam wameanza kazi ya kuvuta waya." Amesema Mhe. Kapinga

Ameongeza kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati inatekeleza miradi ya kupeleka nishati ya umeme kwenye maeneo makubwa ya uwekezaji ikiwemo migodini.

Mhe. Kapinga amesisitiza kuwa makaa ya mawe ni chanzo cha nishati thabiti na ya kutegemewa katika maeneo ya uwekezaji mkubwa hususani viwandani.

Amewapongeza MILCOAL kwa uwekezaji huo ambao unachangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Amewahakikishia wawekezaji kuwa, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi na kuongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inathamini wawekezaji.

Kuhusu Kampuni kuwajibika kwa jamii inayozunguka miradi kwa maana ya CSR, Mhe. Kapinga amesema Sera za Nishati na Madini zinatambua uwajibikaji wa Kampuni kwa jamii zinazozunguka miradi na hivyo ameitaka Kampuni ya MILCOAL kutekeleza suala hilo ipasavyo.

# MGODI WA GGM WAANZA KUTUMIA UMEME WA GRIDI BADALA YA MAFUTA

- Dkt.Biteko azindua kituo cha kupoza umeme cha GGM (MW 34)
- Asema kitaongeza mapato ya mgodi kwa Serikali
- Aipongeza GGM kuzipa kipaumbele kampuni za kizawa
- TANESCO kuingiza mapato ya sh.Bilioni 2 hadi 3 kwa mwezi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amezindua kituo cha kupokea na kupoza umeme katika Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) chenye uwezo wa megawati 34 ambacho sasa kinawezesha GGML kuanza kutumia umeme wa gridi kwa matumizi yake badala ya mafuta na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

Baada ya kuzindua kituo hicho tarehe 13 Agosti 2024 wilayani Geita mkoani Geita, Dkt.Biteko amesema ujenzi wa kituo hicho ni alama halisi ya umoja na ushirikiano uliopo kati ya Serikali na SektaBinafsi kwani mradi huo umehusisha ujenzi wa laini ya umeme ya kV 33 ambayo imejengwa na TANESCO kwa gharama ya shilingi bilioni 8.04 huku GGML ikijenga kituo cha kupoza umeme kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 24.

Amesema GGM ilikuwa inatumia shilingi bilioni 130 kwa mwezi kama gharama za uendeshaji na kwenye umeme wa mafuta ilikuwa inatumia shilingi bilioni 13.4 kila mwezi na kuathiri mapato yake kwa Serikali, hivyo kuanza kazi kwa kituo hicho kunapunguza gharama za uendeshaji kwa mgodi na kupelekea Serikali kuongeza mapato yake, kuongeza ajira na pia GGM kuweza kutanua shughuli zake. Dkt.Biteko ameipongeza kampuni hiyo

kwa kuanza kutumia umeme wa gridi ambao unapunguza gharama za uendeshaji ambapo ametoa angalizo kuwa, kupungua kwa gharama hizo kuguse pia watumishi kwa kuboresha maslahi yao.

Ameeleza kuwa, umeme mwingi unaozalishwa kwa sasa unatoa uhakika wa kwenda kwa wananchi na walaji wakubwa kama GGM na kuweka mkazo kuwa, hayo ni matokeo ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuijali sekta binafsi.

Vilevile, ameipongeza GGM kwa kuzipa kipaumbele kampuni za kizawa katika kutoa huduma kwenye mgodi huo na kusisitiza kuwa huo ndio msimamo wa Serikali ya Tanzania wa kuhakikisha kampuni za ndani zinapewa kipaumbele kwenye miradi mbalimbali.

Dkt. Biteko amewaagiza Watendaji wa Wizara ya Nishati, TANESCO na Taasisi nyingine za Serikali kujali sekta binafsi kutokana na manufaa yake ikiwemo kuwa walipakodi wakubwa na kuongeza ajira nchini.

Pia, amewashukuru watangulizi wake katika Sekta ya Nishati, Dkt. Medard Kalemani na January Makamba ambao katika kipindi chao wakihudumu kama Mawaziri wa Nishati waliusimamia mradi huo ipasavyo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amesema hali ya umeme nchini kwa ujumla ni nzuri huku uzalishaji ukikidhi mahitaji na ziada kidogo.
Kuhusu usambazaji umeme mkoani Geita amesema kuwa Mkoa una Vijiji 486 na kati ya hivyo vijiji 483 vina umeme sawa na asilimia 99.38.

Ameongeza kuwa, kazi ya kupeleka umeme vitongojini mkoani Geita inaendelea ambapo kati ya vitongoji 2,197, vitongoji takriban 1000 tayari vina umeme.
Ameongeza kuwa, Mkoa wa Geita umetengewa Shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kupeleka umeme maeneo ya migodi na viwanda na utekelezaji umefikia asilimia 41.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini ambayo yamepelekea wawekezaji kufanya kazi na kuletea nchi faida akitolea mfano kuwa, katika kipindi cha miaka mitatu GGM imezalisha tani 51 za dhahabu ambayo ni mafanikio makubwa yanayochangia ukuaji wa pato la Taifa.

Amemshukuru Rais Samia kwa kuwezesha umeme kufika pia kwenye migodi ya Wachimbaji wadogo ambapo katika kipindi cha miaka mitatu wachimbaji wadogo 19 wamepelekewa umeme kwenye migodi yao na kuwezesha uzalishaji wa kilo za dhahabu takriban 11,000.

Wabunge mbalimbali waliohudhuria hafla hiyo wamempongeza Rais Samia pamoja na uongozi wa Wizara ya Nishati kwa kutekeleza mradi huo ambao una umuhimu mkubwa kwa uchumi wa nchi na mgodi wenyewe.

# WIZARA YA NISHATI, MTIBWA WAJADILI UJENZI NJIA YA UMEME

- Ni ya msongo wa kilovoti 132
- Ni kufuatia ombi la Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kiwanda cha Mtibwa
- Bilioni 28 kutekeleza miradi ya umeme Vijijini Mvomero



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiongea na wananchi na wafanyakazi wa kiwanda cha Mtibwa, wakati wa ziara yake mkaoni Morogoro alitembelea kiwanda cha Mtibwa na akizindua Bwawa la kumwagilia miwa. Tahehe 03, Agosti 2024.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe amesema, Wizara ya Nishati na Kiwanda cha sukari cha Mtibwa wapo kwenye majadiliano ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 ili kukidhi mahitaji ya Kiwanda cha Mtibwa.

Mhe. Bashe ameyasema hayo leo Agosti 03, 2024 katika ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kiwanda cha Mtibwa alipokuwa akizindua bwawa la kumwagilia miwa.

"Tumefanya kikao kidogo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga kuangalia namna gani umeme mkubwa utafika hapa Mtibwa", na baada ya majadiliano ya kina utekelezaji utaanza'" Amesema Mhe. Bashe.

Ameongeza kuwa majadiliano hayo ya awali yatafungua majadiliano mengine yatakayowezesha umeme waliouomba kiwanda cha Mtibwa kuhakikisha unafika ili kuongeza ufanisi.

Aidha, katika majadiliano ya awali wamekubaliana kutakuwa na makubaliano ya Kiwanda cha Mtibwa kujenga njia hiyo ya umeme kutoka katika kituo cha kupokea na kupoza umeme.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mtibwa Sugar Bw.Seif Ally Seif amesema,mradi wa bwawa una pampu sita kati ya hizo zinazofanya kazi ni pampu mbili kutokana na kutokuwepo kwa umeme wa kutosha,

Aliongeza kuwa njia ya umeme iliyokuwepo ni ya msongo wa

kilovoti 33 huku mahitaji yakiwa njia ya umeme ya msongo 132 hivyo kuweza kwa pampu zote sita kufanya kazi.

Kwa upande wake Mbunge wa Mvomero, Mhe. Jonas Van Zeeland ameishukuru Serikali kwa kuipatia Wilaya ya Kilombero takribani shilingi Bilioni 28 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme Vijijini wilayani humo.

Ameongeza kuwa kati ya Vijiji 60 ambavyo havikuwa na umeme tayari Vijiji 48 vimeshawashwa umeme.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akionge jambo na Kamishina wa umeme na nishati jadidifu Mha. Inocent Luoga wakati wa ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 03 Agosti 2024 katika kiwanda cha Mtibwa alipokuwa akizindua bwawa la kumwagilia miwa.



Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe akiwaeleza wafanyakazi na wananchi makubaliano ya Wizara ya Nishati na Kiwanda cha sukari cha Mtibwa kuhusu majadiliano ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 ili kukidhi mahitaji ya Kiwanda cha Mtibwa.



Wananchi na wafakazi wa kiwanda cha Mtibwa wakisikiliza hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 03 Agosti 2024 katika kiwanda cha Mtibwa alipokuwa akizindua bwawa la kumwagilia miwa.

# KAMATI YA BUNGE YA BAJETI YAAHIDI KUUPA MSUKUMO MRADI WA EACOP

- Yampongeza Rais Samia kutekeleza miradi inayoleta mageuzi ya kiuchumi
- Dkt. Mataragio asema mradi umefikia asilimia 39.2
- Tanzania kufaidika na shilingi trilioni 2.3 kipindi cha ujenzi na uendeshaji
- EACOP yawezesha manunuzi ya USD milioni 462



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti wakiwa katika eneo la Chongoleani wilayani Tanga Mkoa wa Tanga ambapo kunajengwa kituo kitakachotumika kupokea, kuhifadhi na kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti leo wamekagua utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika kituo kitakachotumika kupokea, kuhifadhi na kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda ambapo wameahidi kuzidi kuupa msukumo mradi huo wa kimkakati katika mageuzi ya kiuchumi.

Mara baada ya kukagua kituo hicho kilichopo Kata ya Chongoleani wilayani Tanga, Mkoa wa Tanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Oran Njeza amesema Kamati hiyo ambayo inasimamia mipango na uchumi wa nchi imeona mradi wa EACOP una umuhimu kiuchumi hivyo wataendelea kuupa msukumo mkubwa ili ukamilike kwa wakati.

Kamati hiyo imempongeza, Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mabadiliko ya kiuchumi anayoyafanya kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kama wa EACOP ambayo inaendana na jinsi dunia inavyokwenda kwa sasa.

"Mradi mkubwa kama wa EACOP haukutegemewa kufanyika kwenye nchi za kiafrika lakini maono ya Viongozi Wakuu wa nchi Uganda na Tanzania yamepelekea mradi huu kufanyika ili kuwezesha mafuta sasa kusafirishwa kwa njia ya mabomba ambayo pia yanasaidia katika ulinzi wa mazingira." Amesema Mhe. Njeza

Aidha, Kamati hiyo ya Bajeti imeitaka Wizara ya Nishati kuweka kipaumbele katika ujenzi wa mabomba yakayosafirisha nishati za aina mbalimbali kama vile Gesi na Mafuta na hivyo

kuifanya Tanzania kuwa kituo cha usafirishaji wa nishati hizo barani Afrika.

Vilevile, Kamati imeliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuongeza nguvu ya kuutangaza mradi huo ili wananchi wafahamu jinsi Serikali inavyoendelea kutekeleza miradi yake.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dkt. Batilda Burian amesema kuwa mradi wa EACOP unafaida mbalimbali katika mkoa huo ikiwemo kutoa ajira takriban 900, kuongeza mzunguko wa fedha, kuongeza fursa za biashara ikiwemo katika kituo cha kupokelea, kuhifadhi na kusafirikisha mafuta kilichopo Chongoleani Tanga, kuuza rasilimali kama vile simenti na kupata mapato mbalimbali kupitia ushuru.

Ametilia mkazo masuala ya afya na usalama pahala pa kazi katika miradi mbalimbali nchini ambapo ameipongeza EACOP kwa kutekeleza suala hilo kwa ufanisi ambapo katika masaa zaidi milioni mbili waliyofanya kazi hakuna ajali iliyotokea kwenye maeneo yao ya kazi.

Awali, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio alisema mradi wa EACOP ni wa kielelezo na kimkakati kutokana na faida zake mbalimbali ikiwemo kuongeza mapato ya nchi katika kipindi cha ujenzi na uendeshaji kwa kiasi cha shilingi trilioni 2.3, kutoa ajira kwa watanzania ambapo mpaka leo umeajiri takriban wananchi 7,584 huku ajira hizo zikitarajiwa kuongezeka.

Aliongeza kuwa, kampuni 146 za kitanzania zimehusika kutoa huduma mbalimbali kwenye mradi na kunufaika kwa takriban Dola za Kimarekani milioni 246 na pia mradi umepelekea kufanyika kwa manunuzi ya Dola za Marekani milioni 462 pamoja na vijana wa kitanzania kupata mafunzo ya teknolojia mbalimbali ambapo ujuzi huo watautumia kwenye miradi mingine ya ujenzi wa mabomba kuelekea nchini Kenya na Zambia.

Alitaja wanahisa wa mradi huo kuwa ni Kampuni ya Total Energies ya Ufaransa (62%), CNOOC ya China (8%), Kampuni ya Mafuta ya Uganda (15%) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (15%).

Alisema, kwa ujumla mradi unaendelea vizuri na sasa umefikia asilimia 39.2 huku baadhi ya kazi zikikamilika kwa asilimia 100 huku ujenzi wa kiwanda cha kuwekea mabomba mfumo wa kuhifadhi joto cha Sojo ukifikia asilimia 90 na katika eneo la Chongoleani mradi umefikia asilimia takriban 40 na kueleza kuwa mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2026.

Alieleza kuwa, Serikali inashirikiana vizuri na wanahisa wengine kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na Serikali ya Tanzania imekamilisha kuchangia mtaji wake kama mwanahisa ambapo mpaka leo Serikali.imechangia Dola za Marekani milioni 308 ambayo ni sawa na asilimia 100 ya kiwango ambacho ni cha awali cha gharama za ujenzi kwa asilimia 15 ya hisa za Tanzania.

Kuhusu utwaaji wa ardhi ya mkuza wa EACOP kwa upande wa Tanzania alisema kuwa imekamilika kwa asilimia 99.2 na asilimia iliyobaki inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo masuala ya mirathi. Amesema kuwa kwa upande wa Uganda mradi huo pia unaendelea vizuri.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti wakiwa katika eneo la Chongoleani wilayani Tanga Mkoa wa Tanga ambapo kunajengwa kituo kitakachotumika kupokea, kuhifadhi na kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda.



# RAIS SAMIA AMEFANYA UMEME KUWA SI ANASA- KAPINGA

- Tanzania kufuta historia ya Vijiji kutokuwa na umeme
- Kati ya Vijiji 12,318 bado Vijiji 151 tu kufikiwa na umeme
- Wananchi watakiwa kutunza miundombinu ya umeme




Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amejidhatiti vyema katika kusambaza miradi ya umeme mijini na vijijini na sasa umekuwa si anasa tena kutokana na wananchi kuutumia kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Agosti 16, 2024 wakati akizindua huduma ya umeme katika Kijiji cha Mpingi Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

"Ni dhamira ya Mhe. Rais kuhakikisha Vijiji vyote 12,318 nchini vinapata umeme, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), tumebakisha chini ya Vijiji 151 kuvipelekea umeme na kazi inaendelea." Amesema Mhe. Kapinga

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa Serikali inakwenda kufuta historia ya Vijiji vya Tanzania kutokuwa na umeme kutokana na Vijiji vyote kwenda kufikiwa na nishati hiyo.

Aidha, kutokana na kuelekea kukamilika kwa upelekaji wa umeme kwenye Vijiji, Kapinga amesema sasa Serikali imeelekeza nguvu katika usambazaji wa umeme kwenye Vitongoji.

Amewahakikishia Watanzania kuwa, Serikali itaendelea kupeleka huduma ya umeme katika maeneo yote nchini ili watanzania waweze kuboresha shughuli za kiuchumi.

Awali, Mha. Robert Dulle ambaye ni Msimamizi wa miradi ya umeme vijijini Mkoa wa Ruvuma alitoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa ya uwepo wa umeme kwa kuunganisha kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Aidha, amewaasa wananchi kutunza miundombinu ya umeme hasa kipindi cha utayarishaji wa mashamba ambapo miundombinu mingi huathirika kwa kuchomwa moto.

# SHULE YA SEKONDARI HASNUU MAKAME YAITIKIA AGIZO LA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Mwalimu Mkuu aeleza namna Nishati Safi ya Kupikia ilivyookoa nusu ya gharama
- Aeleza athari zilizopatikana wakati wakitumka nishati isiyo safi




Moja ya maagizo ya Serikali kuelekea katika safari matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia nchini ni taasisi zikiwemo shule kuachana na matumizi ya nishati zisizo safi na salama kama kuni na mkaa wa asili na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ikiwemo gesi.

Shule ya Sekondari ya Hasnuu Makame, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja Visiwani Zanzibar imeanza kutekeleza agizo hilo kwa vitendo ambapo sasa wanafunzi wanafurahia chakula kilichopikwa kwa kutumia nishati safi.


Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Bw. Mohammed Ally anasema matumizi ya kuni shuleni hapo yaligharimu kiasi kikubwa cha fedha na pia kuathiri mwenendo wa masomo kwa wanafunzi.

"Tulilazimika kupeleka wanafunzi hospitali mara kwa mara na maranyingi matatizo makubwa yanakuwa ni ukosefu wa maji kunakosababishwa na kutokula kutokana na chakula kuwa na moshi wa kuni." Anasema Bw. Ally

Anatanabaisha kuwa, wakati Shule hiyo ikianzishwa ilikuwa na Wanafunzi 110 ambapo ilikuwa ikitumia kiasi cha shilingi 650,000/- kila mwezi kwa ajili ya kununua kuni.

Anasema hivi sasa Shule ya Hasnuu ina wanafunzi 471 huku ikitumia shilingi 778,600 kwa miezi miwili kwa ajili ya kununua gesi na kwamba kwa idadi ya wanafunzi ya sasa endapo wangetumia kuni kupikia gharama zingekuwa kubwa zaidi.

Bw. Ally anaeleza kuwa gharama nyingine zilizookolewa kutokana na matumizi ya nishati safi ni gharama za ukarabati wa jiko zilizotokana na kuchakaa kwa sababu ya moshi pamoja na gharama za maziwa kwa Wapishi.






# WIZARA YA NISHATI YASHIRIKI TAMASHA LA KIZIMKAZI ZANZIBAR

- Yatoa huduma moja kwa moja kwa Wananchi kupitia Taasisi zake
- Nishati safi ya kupikia, yawa ajenda ya kuvutia

Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake leo Agosti 21, 2024 zimeshiriki katika Tamasha la Kizimkazi (Kizimkazi Festival) yanayoendelea kwenye kijiji cha kizimkazi wilaya ya Kusini mkoa wa Kusini Kisiwani Zanzibar.




Katika tamasha hilo la Kizimkazi Wizara na taasisi zinatoa elimu ya utekelezaji wa Sera ya Nishati ya mwaka 2015 pamoja na kutoa huduma kwa wananchi hususani katila utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa mwaka 2024-2034.

Katika Banda la Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) wananchi wameweza kujionea moja kwa moja shughuli za uchimbaji wa Gesi Asilia, usafirishaji na uchakataji wake kupitia teknolojia ya Uhalisia Pepe ( Virtual Reality) pamoja na kuelezwa juhudi za Serikali katika uendelezaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

Vilevile, katika banda la Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wananchi wamejionea utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere ( JNHPP) ambao umekuwa kivutio kikubwa kupitia kifaa cha Uhalisia Pepe, sambamba na kutoa elimu juu ya mchango wa Tanesco katika kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya kupikia kwa kutoa elimu ya matumizi bora ya umeme.

Pia, Banda la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wananchi wanapata huduma moja kwa moja za Nishati Safi ya Kupikia kupitia wadau wa usambazaji na waendelezaji wa teknolojia husika, elimu ya usambazaji umeme vijijini na vitongojini na uendelezaji wa miradi ya umeme.


Taasisi nyingine za Wizara ya Nishati zinazoshiriki Tamasha hilo ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ( PURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ambao wanatoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za udhibiti.

Wizara ya Nishati itakuwa na siku maalumu ya Nishati wakati wa Tamasha la kizimkazi ambapo itaendesha Kongamano la Nishati safi ya kupikia na kujumuisha wadau mbalimbali, ambapo mgeni rasmi anatarajia kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko.

Tamasha la Kizimkazi limezinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Agosti 18, 2024 ambapo kauli mbiu ya Tamasha hilo ni ‘‘ Upishi Salama kwa Afya ya Mpishi na kwa Maendeleo ya Jamii”.




LEUM


PETROLEUM
RENEWABLE





WIZARA YA NISHATI